Mamilioni ya vipeperushi vinachapishwa kila mwaka na kugawiwa bure kwa ajili ya kueneza ujumbe wa Islam.

- Katika uchapishaji wa majarida na magazeti, Jumuiya imekuwa ya kwanza katika nchi mbali mbali kuanzisha magazeti ya dini ya Islam.

- Hapa nchini tangu 1936 Jumuiya imekuwa ikitoa gazeti la Kiislam liitwalo ”Mapenzi ya Mungu”.

- Mamia ya misikiti hujengwa duniani na Jumuiya, zikiwemo nchi za Ulaya, America, Australia, Asia na Afrika.

- Katika nyanja za huduma za kijamii, Shirika la Jumuiya liitwalo “Humanity First” (Ubinadamu Kwanza) linafanya kazi ya kuwahudumia wanadamu duniani kote hususan katika bara la Afrika, bila ya kujali dini, rangi, taifa au kabila.

- Kauli mbiu ya Jumuiya itawalayo shughuli zote za Jumuiya ni “**Upendo kwa wote, Chuki si kwa yeyote**.”

Basi njoo ewe mja wa Mungu! Ujiunge na Jumuiyya hii iliyoundwa kwa mwongozo maalum wa Mungu kwa kumtuma Masihi na Mahdi wa zama hizi za mwisho. Jumuiya ipo kwa lengo la kuwaunganisha wafuasi wa dini zote, na wale wasio na dini yoyote, katika udugu mmoja, upendo, amani na maelewano kwa kuwakusanya chini ya bendera ya Mtume Muhammad s.a.w aliye Rehema kwa walimwengu wote.

TOVUTI YETU: www.alislam.org.

**Taarifa za kituo chetu cha**

**MUSLIM TELEVISION AHMADIYYA (MTA)**

ambacho kinafanya kazi muda wote ni:-

**MTA FREQUENCY-12015.V**
**SYMBOL RATE - 29,950**
**SAT SES.5**

**Anuani :-**
Ukiwa na maswali zaidi unaweza kuwasiliana na wabashiri wetu wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya nchini kote, kwa:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Arusha/Kilimanjaro | 0787 770 655 |
| 2. | Dar es Salaam | 0655 105 096 |
| 3. | Dar es Salaam | 0620 124 768 |
| 4. | Dodoma/Singida | 0782 919 298 |
| 5. | Iringa | 0715 884 800 |
| 6. | Kagera | 0716 682 063 |
| 7. | Kigoma | 0716 045 918 |
| 8. | Mara | 0785 676 614 |
| 9. | Mbeya | 0714 266 800 |
| 10. | Morogoro | 0714 601 191 |
| 11. | Mtwara / Lindi | 0656 116 652 |
| 12. | Mwanza | 0788 677 509 |
| 13. | Pwani | 0623 228 033 |
| 14. | Shinyanga | 0788 676 618 |
| 15. | Songea | 0656 116 698 |
| 16. | Tabora | 0788 677 433 |
| 17. | Tanga | 0714 583 380 |
| 18. | Tunduru | 0655 028 203 |
| 19. | Zanzibar | 0675 321 543 |

لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ

**Hapana Apasaye kuabudiwa ila Allah**
**Muhammad ni Mtume wa Allah**

# JUMUIYA YA WAISLAM WA AHMADIYYA

**Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania**
**P.O. Box 376, Dar es Salaam.**
**Mnazimmoja, barabara ya Bibi Titi.**
**Mkabala na Bustani ndogo ya Mnazimmoja**
**Email: ahmusjamtaz@gmail.com**

**Imechapishwa na:**
**Ahmadiyya Printing Press Tanzania**
**Mob: 0715 771 813**
**Email: ahmadiyyaprintingpresstz@gmail.com**

بســـــم الله الـرَّحـمــن الـرَّحــيـــــم

***Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu***

# JUMUIYA YA WAISLAM WAAHMADIYYA

Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya ni taasisi ya kidini ya kimataifa yenye matawi katika nchi 209 duniani kote.

Mnamo mwaka 1889 Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. (aliyezaliwa 1835 na kufariki 1908) alianzisha Jumuiya hii kwa amri ya Mwenyezi Mungu katika kijiji kidogo cha Qadian huko India.

Takriban dini zote kuu zilizopo duniani zinatoa bishara za ujio wa mja mwenye utukufu mkubwa sana katika siku za mwisho kwa namna mbali mbali.

Kwa mfano: Yesu ametabiriwa kuwajia Wakristo mara ya pili, kuwanyakua wateule wa Mungu. Krishna ametabiriwa kuwajia Wahindu, ili kuwarudishia Wahindu ufalme wao. Wakati huo huo, Zoroasta anaaminiwa kuwa atakuja katika siku za mwisho kuja kurudisha tena ufalme wa dini ya Wazoroasta. Kwa kweli, habari kama hizo zipo katika dini kubwa mbalimbali za duniani.

Uislam pia haukukaa kimya katika habari hii bali unatoa bishara ya kudhihiri kwa Masihi Aliyeahidiwa ambaye pia ameitwa Imam Mahdi (Imamu atakayeongozwa na Mwenyezi Mungu) katika zama za mwisho ili kukamilisha ushindi wa dini hii. Mwenye busara akizifikiria bishara hizi kuwa zitimie kila moja bila kuwa na muunganiko wowote na zingine, basi ataona kuwa kutakuwa na watu wengi watakaotokea kwa Mungu na kila mmoja ataitetea dini yake na kuifanya ishinde dini zingine zote. Katika hali kama hiyo, badala ya kupatikana suluhu, mtafaruku na vurugu zitaibuka.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya akitoa utatuzi wa tatizo hili alisema:
“Bishara zote hizi, bila shaka zinamlenga mtu mmoja ambaye atahusiana kwa namna moja au nyingine na dini zote hizi. Atatumwa na Mwenyezi Mungu kuja kuleta suluhu ya kweli duniani na kwa kuwa atakuwa na uhusiano na dini zote hizo, basi watu wa dini hizi wataungana naye, na hitilafu baina yao itaondoka na suluhu itapatikana kwa urahisi.”

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. akiongeza kufafanua alisema:
“Mimi ndiye yule mjumbe wa Mungu niliyekuja kuleta suluhu katika zama hizi za mwisho. Mwenyezi Mungu Amenituma pamoja na ishara zisizopungua elfu kumi, - Amenifanya Bwana Yesu kwa Wakristo, Krishna kwa Wahindu, Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi kwa Waislam”
“Kwa hakika Mungu Hufanya Apendavyo, naye haulizwi bali watu wataulizwa.”
“Ukiniwacha mimi kwingine kote ni giza. Basi nasema kweli kuwa nimekuja kutimiza bishara zote za dini zote kubwa duniani.”
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. hakuleta chochote kipya, bali amekuja kufundisha mafundisho yale yale yaliyotolewa na Mtume Muhammad (s.a.w).

## BAADHI YA SIFA ZA PEKEE ZA JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA

● Jumuiya hii ndiyo pekee miongoni mwa Waislamu ambayo ina kiongozi mmoja duniani ambaye kwa sasa ni Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a.; naye ni Khalifa wa Tano wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.

● Ahmadiyya ni moja kati ya jumuiya ambazo zimekuwa zikikua kwa haraka zaidi ulimwenguni.

● Jumuiya hii ndiyo pekee miongoni mwa jumuiya za kidini za zama hizi inayotumia kila nafasi na fursa kwa nguvu zote katika kuhakikisha kuwa usawa, uadilifu na haki vinatendeka na kustawi na wanadamu wote, popote pale walipo wanapata na kufurahia maisha ya amani na usalama.

● Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu, Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya imejaaliwa kutafsiri Qurani Tukufu katika lugha zaidi ya 71 ikiwemo Kiswahili na Kiyao. Jumuiya imekuwa ya mwanzo kutoa tafsiri kwa Kiswahili tangu Quran ilipoteremshwa kwa Mtume Muhammad s.a.w. Jumuiya inaendelea kuchapisha malaki ya vitabu vya dini Tukufu ya Islam kila mwaka.